



KANISA LA MORAVIAN TANZANIA JIMBO LA KUSINI MAGHARIBI **MBOZI HIGH SCHOOL**



S.L. P 341,
Mbozi – Songwe.

Mobile No- Head Master: 0754-203749

Mobile No- Academic: 0744708354/0764802533

E-mail:mbosec@yahoo.com/ mbozihighschool@gmail.com

FOMU YA MAOMBI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MBOZI AMBAYO NI BWENI NA KUTWA KWA WASICHANA NA WAVULANA MWAKA 2019/2020

Salamu katika jina la Yesu Kristo!

Mpendwa Mzazi, nafurahi kukutaarifu ya kuwa mwanao amekubaliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Mbozi, maarufu kwa jina la “**Mbozi Mission High School**”. Hivyo anakaribishwa sana! tunategemea kuwa mwanafunzi huyu atazingatia sheria na taratibu zote za shule na kuwa atasoma kwa bidii wakati wote.

UTAMBULISHO WA SHULE

Shule ya Mbozi Mission High School inamiliikiwa na Kanisa la Moravian Tanzania-Jimbo la Kusini Magharibi. Ipo umbali wa kilometra saba (7) toka mji mdogo wa Karasha uliopo kando ya barabara itokayo Mbeya kwenda Tunduma. Kituo cha kushukia kinaitwa KARASHA. Kipo kati ya Mji mdogo wa Mlowo na Vwawa.

1. UPATIKANAJI WA FOMU

Fomu hii zinapatikana kwa gharama ya shilingi elfu kumi (Tsh.10, 000) tu pale Jacaranda –Makao Makuu ya Jimbo la Kanisa la Moravian- Jimbo la Kusini Magharibi; Ofisi za Wilaya za kanisa hilo; Usharika wa Nsala – Vwawa; Usharika wa Mwaka – Tunduma na Dar-es-Salaam eneo la Kariakoo (piga simu namba 0756701070 kwa maelekezo zaidi). Pia fomu hizo zinapatikana shulenii, Mbozi High School.

Shule itafunguliwa tarehe 03/01/2019

2. MASOMO YANAYOFUNDISHWA SHULENI

(a) Shule inafundisha masomo ya Sanaa na sayansi ambayo ni General Studies, Kiswahili, Kiingereza, Fizikia,Uraia, Jiografia, Historia, Kemia, Biolojia, Basic Applied Mathematics na Kilimo (Agriculture science). Hivyo aje na Counter book Quire 3 ziwe kumi na moja (08).

(b) Michepuo ni **HGL, HGK, HKL, CBG, PCB** na **CBA** kwa kidato cha tano na sita

2. SIFA

Mwanafunzi awe amepata alama **C** tatu katika masomo yasiyopungua kwenye mtihani wake wa Kidato cha nne. Na kwenye tahasusi (combination) zilizo tajwa hapo juu awe amepata angalau **D**.

Mwanafunzi atakayesoma **PCB,CBG** na **CBA** awe na ufaulu pia wangalau **D**. Hawa watachangia gharama za madawa kwenye maaabara **Tsh, 47,000/=** kwa ajili ya masomo yao kwa vitendo (Practical).

4. ADA NA AKAUNTI NAMBA YA SHULE

Unapolipa ada, zote zipitie benki katika akaunti ya shule iliyopo NMB kwa jina la “**Mbozi Secondary School Replacement**” kwenye akaunti namba **61202300211**.

MAHITAJI MUHIMU YA WANAFUNZI—AJE NAYO SHULENI

(i) **Rimu mbili A4** Kwa ajili ya mitihani kwa mwaka mzimaau ailete moja kwa muhula.

Ada ni kama ifuatavyo:

Tsh. 1,415, 000/= kwa mwanafunzi wa bweni

Tsh. 750,000/= kwa mwanafunzi wa kutwa.

ULIPWAJI WA ADA UTAKUWA KAMA IFUATAVYO

KIDATO CHA V NA VI

	JULAI	SEPTEMBA	JANUARI	APRILI
BWENI	415,000/=	400,000/=	300,000/=	300,000/=
KUTWA	200,000/=	200,000/=	200,000/=	150,000/=

ULIPWAJI WA ADA KWA KIDATO CHA I-IV

	JANUARI	APRIL	JULAI	SEPTEMBA
BWENI	415,000/=	300,000/=	400,000/=	300,000/=
KUTWA	200,000/=	200,000/=	200,000/=	150,000/=

TAFADHALI LIPA ADA/FEDHA HIYO KUPITIA **BENKI AKAUNTI NAMBA IFUATAYO;**

- NMB -- **61202300211** -MBOZI SECONDARY SCHOOL REPLACEMENT

ZINGATIA: HATUTAPOKEA **FEDHA TASLIMU**, HAKIKISHA UMEANDIKA **JINA LA MWANAFUNZI**, NA **KIDATO CHAKE** KWENYE **SLIP YA BENKI** ULIOЛИPIA ADA BENKI.

5. SARE ZA SHULE

(a) WASICHANA

- (i) T- shirt: 2 @ 12,000'== 24,000/= zinapatikana shulen.
- (ii) Sweta: blue uje nayo au Tshs. 10,000 = (sweta la Kenya au India)
- (iii) Chandarua: pembe nne aje nacho
- (iv) Truck suit ya light blue.
- (v) Viatu vyeusi vya kamba vya ngozi vyenye kisigino kifupi pair mbili aje navyo.
- (vi) Mashati mawili 2 Tetron meupe mikono mirefu.
- (vii) Soksi jozi 2 nyeupe ndefu (stocking)
- (viii) Raba rangi ye yote kwa ajili ya michezo.
- (ix) Doti ya kanga au kitenge na nguo za ndani za kutosha, usisahau na ped za kutosha.
- (x) Sketi nne (4) mbili rangi ya damu ya mzee na mbili rangi ya kijani (zingatia kielelezo kilicho ambatanishwa na fomu hii.) sketi iwe ndefu inayozidi magoti yenye malinda madogo madogo.
- (xi) Shamba dress mbili gauni zenye kisolo chini rangi zake ni damu ya mzee (zinapatikana shulen) gharama ni Tshs 15,000/= kila moja.
- (xii) Tai mbili: damu ya mzee na kijani.
- (xiii) Aje na faili moja (spring file) kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake.

NB: Mwanafunzi ambaye atakuja na sare (nguo na viatu) tofauti na hapo juu hatapokelewa.

(b) WAVULANA

- (i) Mashati (2) meupe tetron ya mikono mirefu.
- (ii) Sweta: blue uje nayo (sweta la Kenya au India)
- (iii) Viatu vyeusi vya ngozi na kamba vyenye kisigino kifupi (Pea mbili (2))

- (iv) Soksi jodzi mbili (2) nyeusi ndefu.
- (v) Bukta ya bluu na raba rangi yeyote kwa ajili ya michezo.
- (vi) Chandarua : pembe nne aje nayo au Tshs. 7,000/=
- (vii) T-shirt: 2 @ 12,000/= 24,000/= zinapatikana shulen.
- (viii) Suruali 2: 1 damu ya mzee na 1 nyeusi.

Suruali zishonwe marinda mawili mbele nazisiwe za kubana. Zingatia kielelezo cha kitambaa kilicho ambatanishwa kwenye fomu hii.

- (ix) Shamba dress suruali mbili (2) moja damu ya mzee na moja nyeusi.
- (x) Truck suit ya light blue.
- (xi) Aje na faili (spring file) kwa ajili ya kutunza kumbu kumbu zake
- (xii) Tai mbili: damu ya mzee na nyeusi

NB: Mwanafunzi ambaye atakuja na sare (nguo na viatu) tofauti na hapo juu Hatapokelewa.

6. VIFAA VINGINE,

Kwa wanafunzi wa bweni.

- (i) Tandiko futi 3x6, mashuka jodzi mbili ya pink kwa wasichana na bluu bahari kwa Wavulana, tauko, mto, foronya na blanketi rangi yeyote na yebo yebo.
- (ii) Sahani, bakuli, kijiko, ndoo, iwe rangi nyekundu.
- (iii) Sanduku imara la batu au mbaao.
- (iv) Rula, penseli 3, biki za kutosha, mkebe na karatasi za graph.

7. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Mwanafunzi huruhuswi kufanya yafuatayo:

(a) Taaluma

- (i) Kupiga kelele ukiwa darasani ni marufuku.
- (ii) Kutohudhuria shule muda wa masomo
- (iii) Kuchelewa kurudi shulen baada ya likizo
- (iv) Mwanafunzi hataruhuswi kurudi nyumbani katikati ya muhula pasipo sababu maalum hadi wakati wa likizo.
- (v) Kutoroka mitihani na kazi zingine za darasani
- (vi) Mwanafunzi ambaye atakosa kufanya mojawapo ya mitihani katikati ya muhula, Mitihani ya mihula ya mwisho wa mwaka **HATARUHUSIWA** kuendelea na darasa linalofuata. Iwapo mwanafunzi ni wa kidato cha nne hataruhuswi kufanya mtihani ya Baraza la Mitihani Tanzania.

(b) Nidhamu

- (i) Kufuga kucha ndefu, kusuka nywele, kujichubua usoni.
- (ii) Kufuga ndevu.
- (iii) Kuva mavazi yasiyo na heshima mfano: Suruali mlegezo, nguo za kubana na sketi fupi
- (iv) Kugombana, lugha chafu, matusi mwiko.
- (v) Kuva sketi au gauni fupi – mwenye sketi au gauni fupi ataiharibu nguo hiyo yeye mwenyewe mbele ya wanafunzi ili isitumike tena.
- (vi) Mwanafunzi anayemhifadhi mwanafunzi aliyefukuzwa shule naye atawajibika.
- (vii) Wazazi na wagoni wengine watakuja kuwaona wanafunzi hapa shulen **Jumamosi** ya mwisho wa mwezi kuanzia saa **04.00** asubuhi hadi saa **10.00** jioni. Muda wa mazungumuzo kati ya mgeni na mwanafunzi ni kutoka kwa mwalimu wa zamu.
- (viii) Mwanafunzi asirudi shulen zaidi ya saa **12. 00** jioni la sivyo hatapokelewa.

(c) Chakula.

- (i) Kupiga kelele wakati wa kula chakula.
- (ii) Kuвая ndala ndani Bwalo.
- (iii) Kutumia ndoo na madishi kuchukulia chakula.
- (iv) Kulia chakula Bwenini

NB: Kwa mwanafunzi atakaye kiuka kipengele cha **B** na **C** hapo juu hatua kali sana za kinidhamu zitachukuliwa zidi yote

8. MWANAFUNZI ATAKUWA AMEJIFUKUZISHA SHULE MWENYEWE AKIPATIKANA NA MOJA YA MAKOSA YAFUATAYO:

- (i) Kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa Afisa ye yeyote mwenye mamlaka ye yeyote.
- (ii) Kutokuhudhuria vipindi vya darasani na vya kazi za nje na kutofanya kazi alizopangiwa bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa afisa mwenye mamlaka ya kutoa ruhusa.
- (iii) Wizi.
- (iv) Uasherati.
- (v) Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya.
- (vi) Uvutaji wa bangi na sigara.
- (vii) Makosa ya jinai
- (viii) Kupigana na kupiga.
- (ix) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- (x) Kudharau bendera ya taifa.
- (xi) Kuoa au kuolewa.
- (xii) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani ya nje ya shule
- (xiii) Kutoa mimba.
- (xiv) Kugoma, kuchochea au kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu
- (xv) Kukataa adhabu halali kwa makusudi
- (xvi) Kuwepo katika maeneo yaliyokatazwa mfano: vilabu vya pombe, baa. Majumba ya starehe, kuwepo sehemu za giza mvulana na msichana
- (xvii) Kuвая mavazi yasiyokubalika ndani na nje ya shule wakati mwanafunzi yuko shulenii
- (xviii) Kumiliki au kuwa na simu ya mkononi shulenii.
- (xix) Kutokulipa ada ya shule kwa utaratibu uliopangwa.

KUMBUKA: Shule itafunguliwa na masomo kuanza mara moja tarehe 03 Julai 2018

Nikutakie maandalizi mema na karibu Mbozi High School.

.....
Msyaliha, E .A

MKUU WA SHULE

- A.Jina la Mwanafunzi:.....Mvulana/Msichana
2. Tarehe ya kuzaliwa:.....Mkoa..... 3.
- (i) Jina la mzazi:..... Anuani.....
- (ii) Namba ya simu:.....
- B. 1. Shule ya msingi/sekondari uliyosoma:
- Kata..... Tarafa.....
- Wilaya:.....Mkoa:.....
2. Mwaka uliomaliza Kidato cha Nne:.....
- Mchepuo unaokusudia kusoma kidato cha tano:.....
- C. Uraia:.....Kabila:.....Dini:.....
- D. Mbozi sekondari inautaratibu wakupukutisha wanafunzi wasiofikisha alama zilizowekwa na shule
- E. Shule inamiliwi na Kanisa la Moravian Tanzania Jimbo la Kusini Magharibi.